**Jina…….. Nambari……**

**Shule……**

**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA TATU**

**FASIHI YA KISWAHILI**

**Agosti/Septemba 2013**

**MUDA: SAA 2 ½**

**MTIHANI WA KINDATO CHA NNE- 2013**

***CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI KENYA***

**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA TATU**

**FASIHI YA KISWAHILI**

**Agosti/Septemba 2013**

**muda:saaa 2 ½**

**maagizo**

**Jibu maswali MANNE pakee**

**Swali la kwanza ni la LAZIMA**

**Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne**

**Zilizobaki yaani:Riwaya,ushairi,tamthilia na hadithi fupi.**

**Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja**

***MTIHANI WA PAMOJA WA LAINAKU AGOSTI/SEPT 2013***

## SEHEMU A: FASIHI SIMIULIZI

## (SWALI LA LAZIMA)

1 a) Eleza njia nne za kufanikisha utambaji. (Alama 4)
   b) Nini maana ya nganoa za mtanziko. (Alama 2)
   c) Fafanua wajibu wa visasili. (Alama 8)
   d) Eleza sifa sita za maigizo. (A lama 6)

## SEHEMU B:RIWAYA

## S.A. MOHAMED: *UTENGANO*

2. …Nakimbilia mame chanje ameshaupanaa,ohooooooo,amka.'
   a)Eleza muktadha wa dondoo hii. (Alama 4)
   b)Eleza umuhimu wa mhusika anayerejelewa . (Alama 2)
   c)Maudhui ya mabadiliko yanajitokeza katika riwaya. kwa kutolea mifano **saba,** jadili. (Alama 14)

3. Maisha ya anasa huitumbukiza jamii katika lindi la matatizo. Thibitisha ukwel wa kauli hii huku ukirejea jumuiya ya utengano. (Alama 20)

# SEH EMU C: USHAIRI

Jibu swali la 4 au la 5

**4. soma shairi kisha ujibu maswali**

Mtu wa fikira njema,kwa watu huacha jina
Na watu wajao nyuma,wakapenda kulisoma
Katika dunia nzima likawa kubwa hazina

Na akili si kusema ,Lakini ni kufikiri
Kwa kujua jambo jema,lisilokuwa na shari
mvuka nguo chutama,wendapo wajiadhiri

Na busarani kutenda, tendo ambalo ni jema
Viumbe wakalipenda ,ukapata na heshima
Maisha daima yenda ,utaacha nini nyuma?

Ni roho yenye hekima,usambe ni santuri
Ambayo huweza sema,maneno kwa kukariri
Hali haina uzima,fahamu na tafukuri

Kama akili kunena,tungeshidwa na vinanda
Vya sauti nzuri sana,visivyoweza kutendaq
matendo yenye maana,ambayo mtu hutenda

Fikira ni fani bora ,katika fani za watu
weledi wenye busara,na maarifa ya vitu
Wanafahamu kwa sura,ulimwengu wote watu

**MASWALI**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (Alama 1)
b) Fafanua maadhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili.(Alama 3)
c) Bainisha matumizi matatu ya uhuru wa mashairi katika shairi hili.(Alama 3)
d) Eleza muundo wa shairii hili (Alama 4)
e) Onyesha mbinu mbili za lugha katika shairi hili? (Alama 2)
f) Neno 'jina'lina maana gani katika shairi hili? (A lama 1)
g) Mshairi anatoa tofauti gani kati ya sauti ya santuri,vinanda na sauti ya binadamu? (Alama 2)
h) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

## 5. Mti usio na shina

Shina limeondolewa, ni matawi yabakia,
Hivi mti utakuwa, na matunda kuyatoa,
ningali ninahofia, hatima mbaya yajia,
Mti usio na shina, matawi kuuokoa?

Dharuba naisikia, juu inakotokea,
Gharika nalihofia, chini lajititimua,
mti umening'inia, vipi utajiokoa?
Mti usio na shina, matawi kuuokoa?

Tumaini sijaona, wasiwasi umejaa,
Hapana pa kujibana, wala pa kushikilia,
Labda nguvu ya Rabana, mti ukauokoa
Mti usio na shina, matawi kuuokoa

Wenyewe ulijiono , pekee uliokua,
Na haukushikiria , na jirani walokuwa,
Hapakuwa muamana, kila kitu kuchukua,
Mti usio na shina, matawi kuuokoa?

Kimzani ilituna, kama sio kunona,
Ukiritimba hiyana, ukawa wake mwamama,

Na yanaposhindikana, sasa ni kutafutana,
Mti usio na shina, matawi kuuokoa?

Watu wanamalizana, ngawira kuja gawana,
Huku wajifanya wana, na baba hawakumuona,
Na majina wapeana , ukoo kujulikana,
Mti usio na shina, matawi kuuokoa?

Ila haijajulikana, tufani inavyokazana,
Kama kuna kuokoana, au chini kutupana,
Nani kuagalizana, salamawaje iona,
Mti usio na shina , matawi kuukokoa?

Siwezi zaidi nena, mimi siye ninayejua,
Nahofia mame wana, chakula kutoungua,
Bei kimepanda sana twaweza lala na njaa,
Mti usio na shina , matawi kuuokoa?

**MASWALI**

a) Eleza maana ya kipokeo katika shairi hili. (Alama 2)
b) Mshairi wa shairi hili ana dhamira gani? (Alama 2)
c) Shairi hili ni jazanda.Jadili kwa kotolea mifano mwafaka. (Alama 3)
ii) Jadili mbinu zingine mbili za lugha katika ushairi huu. (Alama 2)
d) Kwa kutolea mifano ,eleza toni ya mshairi (Alama 2)
e) Eleza umbo la shairi kwa kuzingatia ubeti wa kwanza (Alama 4)
f) Fafanua uhuru wa mshairi kwa kutolea mifano mwafaka (Alama 4)
g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye shairi
i)Lajititimua

ii)Kujibana (Alama 2)

# SEHEMU D: TAMTHILIA

## Timothy Arege: Mstahiki Meya

Jibu swali la 6 au la 7

6. (a) Wawakilishi wa wafanyikazi wana majukumu muhimu katika jamii.Jadili majukumu tano. ukirejelea tamthilia ya ***mstahiki meya.*** (Alama 10)
(b) Jadili mbinu hizi za lugha kama zinavyojitokeza katika tamthilia mstahiki meya.
i) Taharuki
ii) Utatu (Alama 10)

7) Ufisadi ni kikwaza kikubwa katika nchi zinazoendelea.Kwa kurejelea tamthilia mstahiki meya,jadili huku ukionyesha athari zake. (Alama 20)

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

## K. Walibora na Said A. Mohamed: *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

8) Fafanua maudhui ya umaskini na athari zake katika hadithi; (Alama 20)
   i) Mwana wa darubini
   ii) Ndoa ya samani.
   iii) Kanda la usufi.
   iv) maskini ,Babu yangu.